JARIBIO LA MTIHANI

DARASA LA NANE - MWAKA 2019

KISWAHILI:LUGHA

STEP FLYER 001

8

SEHEMU YA KWANZA :LUGHA *Muda: Saa 1 Dakika 40*

SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI

1. Umepewa kijikaratasi hiki cha maswali na karatasi ya majibu. Kijikaratasi hiki kina maswali 50.
2. Katika karatasi ya majibu hakikisha umeandika:-
   (i) Jina lako *(ii) Jina la shule yako*

Kifungu kifuatacho kina nafasi 1 hadi 15. Chagua jibu lililo bora zaidi kujaza pengo.

Alijaribu kuwa ____1____ pia kuwa ____2____ kwamba mambo ____3____ hufanywa kwa ____4____ lakini hawakuweza ku____5____. Ndugu wakaingiwa na ____6____ na wazee nao waka ____7____ juu ya ____8____ hao wawili wasiotaka ku ____9____ madhara yatakayowakabili wasipotaka ku____10____.

1.	**A.** bainisha	**B.** fafanulia	**C.** fahamisha	**D.** potosha
2.	**A.** sihi	**B.** rai	**C.** bembeleza	**D.** kemea
3.	**A.** duni	**B.** aali	**C.** adhimu	**D.** bora
4.	**A.** pupa	**B.** asteaste	**C.** polepole	**D.** taratibu
5.	**A.** afikiana	**B.** elewana	**C.** kubaliana	**D.** shutumiana
6.	**A.** wahaka	**B.** fazaa	**C.** buraha	**D.** hofu
7.	**A.** foka	**B.** ghadhibika	**C.** hamaki	**D.** tabasamu
8.	**A.** wandani	**B.** hasimu	**C.** sahibu	**D.** marafiki
9.	**A.** tadbiri	**B.** vumilia	**C.** pima	**D.** zingatia
10.	**A.** patanishwa	**B.** suluhishwa	**C.** sikizanishwa	**D.** zozanishwa

Watazamaji ____11____ mechi baina ya timu hizo mbili ambazo ____12____ kwani zilienda sare ____13____. Lakini alipopiga ____14____ papo hapo vurumai ikaanza, kukawa pata ____15____.

11.	**A.** walishangaa	**B.** walishangilia	**C.** walishangiza	**D.** walishangaza
12.	**A.** hazikufungana	**B.** hazikufunga	**C.** hazikufungwa	**D.** hazikufuniana
13.	**A.** tosha	**B.** sufuri	**C.** bila	**D.** tasa
14.	**A.** hatua	**B.** kofi	**C.** kipenga	**D.** mayowe
15.	**A.** pata	**B.** chako	**C.** ulipatalo	**D.** shika

Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.

16. Ni methali ipi yenye maana sawa na:
Bendera hufuata upepo.
A. mwenye macho haambiwi tazama.
B. mpanda ngazi hushuka.
C. maji hufuata mkondo.
D. damu ni nzito kuliko maji.

17. Udogo wa **mbuzi** ni
A. kijimbuzi
B. jibuzi
C. kibuzi
D. kimbuzi

18. Nafasi iliyotengenezwa ukutani kuwekea vitu ni:
A. shubaka
B. rafu
C. pazia
D. dari

19. Hili ni umbo gani?



A. Nyota
B. Sayari
C. Kipenyo
D. Hilali

20. Ni sentensi ipi yenye **ki** ya kielezi.
A. jazia ya ihsani ni ihsani
B. ya mkiwa haizai nyike
C. watende wao, wakitenda wenzi wao iwe mwao
D. sicheze na tazo itakuvuaza

21. Kazi yangu ni kuwatetea washtakiwa mahakamani, mimi ni?
A. Hakimu
B. Wakili
C. Karani
D. Mhariri

22. Utamwitaje ndugu wa kike wa mumeo?
A. Ami
B. Mwamu.
C. Umbu
D. Wifi.

23. Chagua wingi wa sentensi:
Hakudhania kwamba nitamshinda
A. Hawakudhania kwamba tutawashinda.
B. Hawakudhania kwamba nitamshinda.
C. Hawakudhania kwamba ningemshinda.
D. Hawakudhania kwamba tutamshinda.

24. Mtu akikuambia "alamsiki." utamjibu?
A. Buheri.
B. Binuru.
C. Hongera.
D. Makiwa.

25. **Andika kinyume cha sentensi ifuatayo:**
Baba atarudi kesho asubuhi
A. Baba hatarudi kesho asubuhi.
B. Mama aliondoka jana jioni.
C. Mama aliondoka jana Asubuhi.
D. Baba hataondoka kesho asubuhi.

26. **Andika tarakimu:**
Milioni sabini na saba, mia tatu na tano elfu mia sita na sita
A. 773 005 606
B. 707 305 606
C. 77,305 606
D. 7 735 606

27. **Uhabeshi ni:**
A. Ethiopia
B. Malawi.
C. Ghana
D. Eritrea

28. Lo! lile ni joka kubwa sana Neno **Lo!** ni
A. kionyeshi
B. kiulizi
C. kisisitizi
D. kihisishi

29. Piga moyo konde ni:
A. kujiua
B. kujipiga msasa
C. kujikaza
D. kujidhulumu

30. Hakimu wa kiislamu huitwaje?
A. Jaji.
B. Kadhi.
C. Mwadhini.
D. Sheikh.

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31-40

Kiwanda cha umoja cha kutengenezea viatu vya aina ya ndara kilichoko Mtwapa, Kaskazini mwa Mombasa, kimekuwa na maendeleo mazuri kwa sababu ya usimamizi mzuri, jitihada za wafanyikazi na ubora wa viatu vyake,

Ajabu ni kwamba kiwanda hiki kilifunguliwa miaka mitano tu iliyopita lakini kwa siku moja kinaweza kutengeneza viatu jozi elfu kumi na tatu na mia tatu. Pia inasemekana kwamba kwa mwezi kiwanda hicho kinaweza kutoa zaidi ya viatu jozi laki tatu na elfu tisini na tisa. Ubora wa viatu vyenyewe vimefanya viatu hivyo viuzike kwa urahisi hata nchi za ng'ambo kwani kizuri chajiuza chenyewe.

Marupurupu wanayopewa wafanyikazi, ni moja kati ya motisha zinazotumika kiwandani. Matibabu na elimu ya watoto wa wafanyakazi hao, pia hushughulikiwa vilivyo. Ndiposa wafanyakazi hao, wasiopungua dazeni kumi na mbili, wako tayari kufanya kazi usiku na mchana pindi wanapotakiwa kufanya hivyo, kwani wanajua kwamba "Ushikwapo shikamana."

31. Viatu vya ndara ni viatu vya
A. kijeshi
B. kanda mbili
C. kutembelea
D. wanawake

32. Sababu zinazofanya kiwanda cha umoja kufaulu ni
A. 3
B. 4
C. 5
D. 6

33. Kiwanda cha umoja
A. kiko kusini mwa Mombasa
B. kina wafanyikazi mia tano
C. kinatoa viatu aina nyingi
D. kinauza viatu hata nchi nyinginezo

34. Kwa mwezi kiwanda hiki kinatengeneza viatu
A. 399,000
B. ~~39900~~
C. 309, 900
D. 3990000

35. Maliza methali
Kizuri chajiuza
A. kwa bei nzuri
B. kwa bei ghali
C. na watu hukipigania
D. kibaya chajitembeza

36. Idadi ya wafanyikazi kiwandani ni
A. 12
B. 102
C. 144
D. 13,300

37. Marupurupu ni malipo ya juu juu. Pesa anazotozwa mtu kwa kumtoa damu mwingine zinaitwa
A. karadha
B. fichuo
C. kiokozi
D. arshi

38. Sababu inayowafanya wafanyakazi wa kiwanda hicho kuwa tayari kufanya kazi usiku na mchana ni
A. kule kutazamwa vizuri
B. kutaka pesa zaidi
C. kuogopa kushikwa wakigoma
D. kwa kuwa ni wengi

39. Viatu vya kiwanda hiki vinauzika kwa wingi kwa sababu
A. wafanyakazi ni wengi
B. Bei yake ni rahisi
C. viatu vyenyewe ni vizuri
D. vinauzika huko ng'ambo

40. Maana ya methali "Ushikwapo shikamana," ni
A. ukishikwa usibishane, kubali
B. ukishikwa shindana, usikubali
C. usikubali kushikwa ovyoovyo
D. unaponufaishwa patunze

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali 41-50

Moyo wanambia penda, mtu mjinga sipende,
Mjinga ukimpenda, hajui nini atende,
Moyo wanambia tenda, lisilo tendwa sitende,
Fanya wanavyotenda, wenzio wasikushinde.

Moyo wanambia imba, wimbo mbaya siimbe,
Imba wimbo wa kupamba, uwa pambaze wakembe,
Moyo wanambia omba, ombi ovu usiombe,
Omba Mungu muumba, dhiki asifanye chembe.

Moyo wanambia meza, kinachokwama simeze,
Kinachokwama kumeza, kinywani sielekeze,
Moyo wanambia uza, roho yake usiuze,
Fanya unavyoweza, neno hili jikataze.

Moyo wanambia cheza, michezo mbi sicheze,
Cheza wa kupendeza, wenzio wakuigize,
Moyo wanambia kaza, bidii usipunguze,
Usipunguze kuwaza, mawazoni jiingize.

Moyo wanaimbia kana, neno la kweli sikane,
Kweli unapoiona, fanya bidii unene,
Moyo wanambia chuna, ngozi yako usichune,
Japo nyeusi sana, bora kuliko nyingine.

41. Katika ubeti wa kwanza
A. moyo wamkanya mtunzi kumpenda mjinga.
B. Moyo wamkanya mtunzi asimpende mjinga.
C. Moyo wanambia mtunzi atende kama wenzake.
D. Mtunzi asema ukimpenda mjinga, hujui unachofanya.

42. Mtunzi anasema
A. wimbo mbaya unaweza kukutanda
B. umwimbie Mungu muumba
C. meza kila kinachoweza kukusakama
D. uendeleze uwezo wa kufikiri na kutafakari

43. Mshairi anasema kwamba
A. kucheza kuwe bora
B. bora kucheza
C. fanya bidii uwe mnene lakini usichune ngozi
D. kana neno lolote

44. Shairi hili ni la aina ya_____
A. tathlitha B. taklimisa
C. tarbia D. tathnia

45. Kifungu kimoja cha shairi huitwa
A. mshororo B. mizani
C. kibwagizo D. ubeti

46. Kibwagizo cha ubeti wa nne kina mizani mingapi?
A. 16 B. 15
C. 4 D. 8

47. Chagua mpangilio sahihi wa vina vya kati na vya mwisho katika ubeti wa tatu wa shairi hili
A. za-ze B. nda-nde
C. na-ne D. mba-mbe

48. Kwa mujibu wa shairi, neno makembe ni sawa na
A. wazembe B. watoto
C. watu D. wapumbavu

49. Bingwa wa kutunga nyimbo huitwa manju, naye bingwa wa kutunga mashairi huitwa
A. sogora B. manju
C. malenga D. mutribu

50. Anwani mwafaka kwa shairi hili ni
A. Moyo
B. Manju
C. Moyo wanambia
D. Moyo wanambia panda